**KISWAHILI**

**Tarehe: 19/Juni/2025**

**Wakati: 14h00’-16h00’**

NESA NATIONAL EXAMINATION AND SCHOOL INSPECTION AUTHORITY

# MWONGOZO WA KUKOSOA MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA TATU

**KIWANGO:** **Kidato cha Kwanza**

**MUDA:** **Masaa mawili (2)**

**ALAMA:** **...... /20** **CAMIS:** **...... /20**

**MAELEKEZO**

- **Usifungue karatasi hii ya mtihani bila ruhusa.**
- **Mtihani huu unaundwa na sehemu kuu mbili:**
  - **Sehemu ya I: Ufahamu (alama 5),**
  - **Sehemu ya II: Sarufi na matumizi ya lugha (alama 15).**
- **Mtihani huu unaundwa na maswali 10.**
- **Jibu maswali yote kulingana na maelekezo yaliyotolewa.**
- **Tumia kalamu ya bluu au kalamu nyeusi.**
- **Kuhusu maswali ya kuchagua, weka mduara (0) kwenye herufi ya jibu lililo bora.**

**SEHEMU YA I: UFAHAMU (ALAMA 5)**

**Soma kifungu cha habari kinachofuata kisha ujibu maswali yanayofuata:**

**Usafi shuleni**

Mimi ni Mutoni. Shule yangu inaitwa Bwiza. Sasa ni wakati wa kufanya usafi shuleni. Wanafunzi wa darasa la kwanza wanachukua majembe ili kusafisha na kutengeneza bustani iliyo karibu na shule. Mimi na Kayitare tunasafisha vyoo. Aisha, Kabera na Marita wanafagia darasani. Mutesi na Muhire wanasaidia wengine kusafisha darasa letu. Shule yangu ina wanafunzi wavulana na wasichana. Wote husaidiana katika shughuli zote za usafi. Wakati wa mvua tunapanda miti na maua karibu na shule.

Mugabe na Musa wanasoma katika shule ya Kimira. Shule yao ni chafu sana.

Shule hii ina wanafunzi wavivu sana. Wao hutupa takataka popote. Wao hawasafishi madarasa yao na hawafui sare zao za shule. Wao hawachunguzwi vizuri na walimu wao na hawajali umuhimu wa usafi. Kweli, magonjwa huwashika mara kwa mara.

Maswali ya ufahamu

**Kuhusu maswali ya kuchagua, zungusha mduara (0) kwenye herufi ya jibu lililo bora.**

1) Shule ya Mutoni inaitwaje? **(alama1)**
   a) Kimira
   b) **Bwiza**
   c) Kinihira
   d) Bwira
2) Wanafunzi wa darasa la kwanza wanachukua nini kufanya usafi? **(alama1)**
   **a) Majembe**
   b) Visu
   c) Miti

d) Mapanga

3) **Mutoni na Kayitare wanasaidia kufanya nini?** **(alama1)**

**a)** Kufagia madarasa

**b) Kusafisha vyoo**

**c)** Kupandisha miti

**d)** Kutoa nyasi

4) **Shule ya Mugabe na Musa inaonekana vipi?** **(alama1)**

a) Ni safi sana

b) Ina kubwa sana

**c) Ni chafu sana**

d) Ina wanafunzi wengi

5) **Ni somo gani unalojifunza kutokana na kifungu cha habari umekisoma hapo juu?** **(alama1)**

a) Kuwa na uvivu kwa ajili ya kusoma vizuri.

**b) Kuwa na usafi kwa ajili ya kujilinda magonjwa yanayotokana na uchafu.**

c) Kuwa na uchafu kwa ajili ya kusababisha magonjwa

d) Kutokuwa na usafi kwa ajili ya kusababisha magonjwa yanayotokana na uchafu.

**SEHEMU YA II: SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA** **(alama 15)**

6) Mtoto wa kiume huitwa: **(alama 3)**

a) Msihana

**b) Mvulana**

c) Mke

d) mzee

7) Chagua nafsi inayofaa kujaza sentensi ifuatayo: **(alama 2)**

-…………………amefika nyumbani.

a) Mimi

b) Sisi

c) **Yeye**
d) Ninyi

8) Husisha kifaa kutoka katika sehemu A na umuhimu wake katika sehemu B. **(alama 4)**

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| Kijiko | Kuoga |
| Dirisha | Kulia chakula |
| Sabuni | Kulala juu yake |
| Kitanda | kuingiza hewa nyumbani |

| **Sehemu A** | **Sehemu B** |
|---|---|
| **Sabuni** | **Kuoga** |
| **Kijiko** | **Kulia chakula** |
| **Kitanda** | **Kulala juu yake** |
| **Dirisha** | **kuingiza hewa nyumbani** |

9) Tunga sentensi yako mwenyewe kwa kutumia neno lililopigwa mstari. **(alama 4)**

a. Bei ya chumvi imepunguka siku hizi.
b. Mimi naenda kununua kalamu.

**Mfano:**

**a. Viatu hivi nilivinunua kwa bei ndogo saba**

**b. Naenda sokoni kununua viazi vitamu**

10) Panga vizuri maneno yafuatayo ili utunge sentensi yenye maana: **(alama1)**

- ina yangu mia Shule mbili wanafunzi

**Shule yangu ina wanafunzi mia mbili**

**Mwisho.**